**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS - MIPANGO NA UWEKEZAJI**

# MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), AKIWASILISHA KWENYE MKUTANO WA WABUNGE WOTE MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27.

**11 MACHI 2026**

**MAELEZO YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHESHIMIWA PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB), AKIWASILISHA KWENYE MKUTANO WA WABUNGE WOTE MAPENDEKEZO YA SERIKALI YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2026/27**

---

## UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa kuzingatia Kanuni ya 119 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kuwasilisha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/2027.

**2.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Ninaomba nianze maelezo yangu kwa kumshukuru Mungu kwa kututunza katika kipindi chote tangu tulipoachana katika mkutano uliopita na kuturudisha salama. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Musa Azan Zungu (Mb.), Spika wa Bunge la Tanzania kwa kuendelea kuratibu shughuli za Bunge na kuliongoza Bunge letu kwa umakini na umahiri mkubwa.

**3.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27 unaopendekezwa ni sehemu ya nyenzo muhimu katika

kutekeleza Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 20230/31 ulioidhinishwa na Bunge lako Tukufu katika mkutano wake wa pili uliofanyika kuanzia tarehe 27 Januari hadi tarehe 06 Februari 2026.

**4.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kitabu cha Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 kinawasilishwa katika sura saba (7). ***Sura ya Kwanza*** ni utangulizi ukijumuisha usuli, malengo, na mawanda ya Mpango. ***Sura ya Pili*** ni mapitio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2024/2025 na mwelekeo wa hali ya Uchumi kwa mwaka 2026/2027. ***Sura ya Tatu*** ni tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, ambao muda wake wa utekelezaji unakamilika mwezi Juni 2026. ***Sura ya Nne*** inawasilisha vipaumbele kwa mwaka 2026/27. ***Sura ya Tano*** inawasilisha ugharamiaji wa Mpango. ***Sura ya Sita*** inaainisha mikakati ya ufuatiliaji na tathmini. ***Sura ya saba*** inabainisha vihatarishi katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, Kitabu kina viambatishi viwili. ***Kiambatisho Na.1*** ni Mwenendo wa Viashiria vilivyotumika katika Upimaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa 2021/22 – 2025/26, na ***Kiambatisho Na. 2*** ni Orodha ya Miradi ya Maendeleo ya kKpaumbele kwa Mwaka 2026/27.

## HALI YA UCHUMI

**5.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Januari 2026, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2025 kama ilivyokua kwa mwaka 2024, ikilinganishwa na asilimia 3.5 mwaka 2023. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia inatarajia kuendelea kubaki wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2026 na kupungua hadi asilimia 3.2 mwaka 2027. Ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2026/27 unatarajiwa kuchagizwa na kuathiriwa na mabadiliko ya sera za biashara, uwekezaji katika teknolojia, hususan teknolojia ya akili unde (AI), na migogoro na vita zinazoendelea katika sehemu mbalimbali duniani, hususani nchini Ukraine na mashariki ya kati.

**6.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara (*sub-Saharan African countries*) uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 4.1 na 3.7 mwaka 2024 na 2023 mtawalia. Kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi kulichangiwa na kupungua kwa athari za majanga yanayokabili uchumi wa dunia, kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kufuatia ongezeko la uwekezaji katika sekta ya umma, kuimarika kwa mauzo ya bidhaa nje na utekelezaji mzuri wa sera

za kupunguza mfumuko wa bei. Ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoko kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kuongezeka hadi kufikia asilimia 4.6 mwaka 2026 na 2027, ukichangizwa na juhudi za kuimarisha uchumi jumla na mageuzi ya sera za kiuchumi katika nchi za eneo hili.

**7.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uchumi ulikua kwa wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 3.8 mwaka 2023 na unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 na asilimia 3.7 mwaka 2025 na 2026, mtawalia. Kwa upande wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ukuaji wa Pato la Taifa ulikua kwa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024 ikilinganishwa na asilimia 5.3 mwaka 2023. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi wa ukanda wa EAC ilichangiwa na kuporomoka kwa uchumi wa nchi ya Sudani Kusini iliyoshuhudia ukuaji hasi wa asilimia 26.1 mwaka 2024. Uchumi wa nchi za EAC unakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 7.7 mwaka 2025 na mwaka 2026.

**8.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Januari 2026, mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi kutokana na utekelezaji wa sera za fedha zilizolenga kuwa na utulivu wa mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kupungua kutoka wastani

wa asilimia 5.6 na 4.1 kwa mwaka 2024 na 2025 mtawalia hadi asilimia 3.8 mwaka 2026 na 3.4 mwaka 2027.

**9.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kwa upande wa Tanzania, katika kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka 2025, ukuaji wa Pato la Taifa kwa bei za mwaka wa kizio wa 2015 ulifikia wastani wa asilimia 6.0 ikilinganishwa na asilimia 5.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Ukuaji huo ulichochewa na uwekezaji wa Serikali katika miradi ya kimkakati ya miundombinu ya nishati, maji, na usafirishaji; kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji hususan kilimo, viwanda na uchimbaji wa madini na mawe; pamoja na kuendelea kuimarika kwa sekta ya fedha na shughuli za usafirishaji nchini.

**10.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mwaka 2025, mfumuko wa bei nchini ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 ikilinganishwa na asilimia 3.1 mwaka 2024. Kiwango hicho cha mfumuko wa bei kipo ndani ya lengo la nchi la muda wa kati la asilimia 3.0 hadi 5.0, vigezo vya mtengamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (usiozidi asilimia 8.0) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (wigo wa asilimia 3.0 hadi 7.0).

## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25 NA NUSU YA KWANZA YA MWAKA 2025/2026

**11.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** hadi kufikia Desemba 2025, Serikali imeendelea kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za kimkakati ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Utekelezaji wa miradi hiyo umechangia kuimarika kwa sekta za miundombinu, nishati, kilimo, viwanda, madini, utalii na huduma za jamii, na hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi pamoja na ustawi wa wananchi.

**12.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo:

i) **Kuendelea kuimarisha sekta ya kilimo**, ikiwemo utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji na ukuzaji wa mazao ya kimkakati kama pamba, korosho, kahawa na nafaka ili kuongeza uzalishaji na kuimarisha usalama wa chakula;

ii) **Kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa umeme**, kupitia miradi mikubwa ya nishati ikiwemo Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa

Julius Nyerere na miradi ya gesi asilia ya Kinyerezi, hatua iliyosaidia kuongeza upatikanaji wa nishati kwa viwanda na shughuli za kiuchumi;

iii) **Kuboresha miundombinu ya huduma za jamii**, hususan elimu kwa kupanua fursa za upatikanaji wa elimu ya msingi na sekondari bure pamoja na kuboresha miundombinu ya shule na mafunzo ya walimu;

iv) **Kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira** vijijini na mijini kwa lengo la kuboresha afya za wananchi na kupunguza magonjwa yanayotokana na maji yasiyo salama;

v) **Kutekeleza programu za kupunguza umaskini,** ikiwemo programu za TASAF zinazolenga kuongeza kipato cha kaya maskini na kukuza ajira;

vi) Kuimarisha **miundombinu ya usafiri na usafirishaji**, ambapo matumizi ya reli yameongezeka na kusaidia kupunguza gharama na muda wa usafiri pamoja na kuchochea biashara na utalii.

**13.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango huo ni pamoja na:

- kuongezeka kwa shehena ya mzigo iliyosafirishwa kwa reli kutoka tani 484,673 mwaka 2023/24 hadi tani 531,359

mwaka 2024/25;

- kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kutoka MW 4,032 mwaka 2024/25 hadi MW 4,504.54 mwaka 2025/26;
- kuongezeka kwa kiwango cha uandikishaji rika lengwa katika elimu ya awali kutoka asilimia 40.5 mwaka 2023/24 hadi asilimia 51.2 mwaka 2024/25;
- kuongezeka kwa miundombinu ya usambazaji wa maji vijijini, ambapo idadi ya watu vijijini waliofikiwa na mtandao wa maji safi na salama imeongezeka kutoka asilimia 83 mwaka 2024/25 hadi asilimia 85.6 mwaka 2025/26;
- Kuongezeka kwa idadi ya watalii wa ndani na nje kufikia 5,905,455 mwaka 2025/26 ikilinganishwa na watalii 5,360,247 mwaka 2024/25; na
- kuongezeka kwa eneo la umwagiliaji kufikia hekta 983,466.6 mwaka 2024/25 ikilinganishwa na hekta 727,280.6 mwaka 2023/24.

## MAENEO YA KIPAUMBELE KWA MWAKA 2026/27

**14.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mwaka huu tunaanza rasmi kutekeleza Dira 2050, inayolenga kujenga **Taifa Jumuishi, Lenye Ustawi, Haki na Linalojitegemea.** Kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji wa Dira 2050, Serikali iliandaa nyenzo mbili muhimu ambazo Bunge lako hili liliziidhinisha katika Mkutano wake wa Pili. Nyenzo hizi ni Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (*Long-Term Perspective Plan – LTPP 2050*) na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 (*Fourth Five Year Development Plan – FYDP IV*).

**15.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Hivyo basi, vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27 vimeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele, malengo, shabaha, afua na viashiria muhimu vya utendaji vilivyoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31. Mpango huu unaongozwa na dhima ya *"**Mageuzi kwa ajili ya Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira**",* na ni wa kwanza katika utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu 2026/27 – 2050/51 na Dira 2050.

**16.** Katika kutekeleza dhima ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 ya *"**Mageuzi kwa ajili ya***

***Ukuaji Jumuishi wa Uchumi na Uzalishaji Ajira",*** katika mwaka 2026/27, mageuzi yataelekezwa katika maeneo nane yafuatayo:

i) Kufanya mageuzi ya mifumo na utawala bora ili kujenga msingi wa utawala bora, uwazi na ufanisi;

ii) Kufanya mageuzi ya kiuchumi yanayolenga usimamizi wa uchumi ili kuongeza wigo wa ukuaji wa sekta za uzalishaji zikiwemo kilimo, viwanda, huduma na uchumi wa kidijitali;

iii) Kufanya mageuzi ya sekta ya nishati katika sera na mifumo ili kukidhi mahitaji ya umeme nchini;

iv) Kuimarisha maandalizi ya miradi (Project Preparation) ili kuhakikisha inakidhi vigezo vya kifedha, kiuchumi na kisheria vinavyohitajika kuvutia wawekezaji.

v) Kuendeleza Mkakati wa Miradi ya PPP (PPP Pipeline): Kuandaa na kusimamia orodha ya miradi ya kimkakati inayoweza kutekelezwa kwa PPP katika sekta za kipaumbele kama nishati, usafiri na usafirishaji, miundombinu ya maji, TEHAMA, viwanda na maendeleo ya miji;

vi) Kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji: Mageuzi ya kisheria na kiutawala yataendelea ili kupunguza urasimu, kuongeza uwazi na kuimarisha utabirikaji wa kisera, hatua ambazo ni muhimu kwa kuongeza imani ya wawekezaji;

vii) Kutumia mwongozo wa kitaifa wa upangaji: Mwongozo huu unahakikisha sekta zinaandaa mipango mikakati yake kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2026/27 – 2030/31 pamoja na Dira 2050; na

viii) Kuendelea kufanya mageuzi ya mashirika ya umma ili kuongeza mchango wake katika uwekezaji na kuunganisha baadhi ya mashirika ili kuongeza ufanisi.

**17.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** matokeo yanayotarajiwa kutokana na utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Mwaka 2026/27 ni pamoja na:

i) Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa pato la Taifa kufikia asilimia 6.3 mwaka 2026;
ii) Mfumuko wa bei kuendelea kuwa wigo wa asilimia 3.0 - 5.0;
iii) Kuongezeka kwa mapato ya kodi kufikia asilimia 13.7 ya pato la taifa;
iv) Kuongezeka kwa uzalishaji wa ajira kufikia 1,700,000 mwakas 2026/27 (ukilinganisa na ajira 981,000 zilizozalishwa mwaka 2024/25) katika sekta za kilimo, uzalishaji viwandani na huduma (utalii, biashara, usafiri, n.k.);
v) Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme kufikia MW 4,654.5 (ukilinganisha na MW 4,504.54 mwaka 2025/26);
vi) Kuongezeka kwa eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni 1.2 (ukilinganisha hekta 980,000 mwaka 2024/25); na
vii) Kuongezeka kwa mizigo inayosafirishwa katika reli kufikia tani 810,000 (ukilinganisha na tani 531,359 kwa mwaka 2024/25).

**18.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Gharama ya kutekeleza Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ili kufikia malengo yaliyowekwa inakadiriwa kuwa TZS trilioni 477.747. Kati ya fedha hizi, asilimia 70 (trilioni 324.487) inatarajiwa kutoka katika sekta binafsi, na asilimia 30 (trilioni 153.26) kutoka katika sekta ya umma (serikali kuu, serikali za mitaa na mashirika ya umma).

**19.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Gharama za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/2027 zinakadiriwa kuwa TZS trilioni 86.3 (sawa na asilimia 18.1 ya gharama za kutekeleza Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano). Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27 unatarajiwa kutekelezwa na wadau wakubwa watatu: serikali kuu na mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi na mashirika ya umma.

**20.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Sekta binafsi inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 60.1 (sawa na asilimia 69.6). Sekta ya umma kwa ujumla wake inatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 26.2 (sawa na asilimia 30.4), ambapo mashirika ya umma yanatarjia kuchangia shilingi trilioni 5.5. Serikali itachangia shilingi trilioni 20.7, itakayotengwa kutoka katika Bajeti Kuu ya Serikali ya shilingi trilioni 62.3, (sawa na asilimia 33.3 ya bajeti kuu ya serikali).

**21.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, Serikali inapendekeza kutekeleza maeneo ya kipaumbele matano kama yalivyoanishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano kama ifuatavyo:

i) *Kuimarisha Utawala Bora, Demokrasia, Amani, na Utulivu*

ii) *Kujenga Uchumi Imara, Jumuishi na Shindani*

iii) *Kuimarisha Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii*

iv) *Kuimarisha Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu kwa Mabadiliko ya Tabianchi*

v) *Vichocheo vya Mageuzi (ikiwemo nishati, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, utafiti na maendeleo, na mageuzi ya kidigiti).*

**22.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Katika kutekeleza maeneo ya vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Serikali imepanga kutekeleza programu na miradi 408 **(Kiambatisho 2),** ikiwemo miradi shikizi 38 iliyopo katika programu saba za kielelezo zilizoainishwa katika Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**23.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Mashirika ya umma yanatarajiwa kutekeleza programu na miradi itakayopunguza ruzuku kutoka serikalini na kupunguza hasara, kuanzisha bondi za makampuni (corporate bonds), *asset monetisation*, kuunganisha baadhi ya mashirika ya umma ili kuongeza ufanisi, na kuwezesha mashirika ya umma kuingia katika masoko ya hisa ili kuongeza ushiriki wa wananchi katika kukuza mitaji. Aidha, mashirika ya umma yanatarajiwa kuwekeza katika sekta mbalimbali, zikiwemo za nishati, usafiri na usafirishaji, kilimo, afya, miliki, utalii, mawasiliano, madini, huduma, na uzalishaji viwandani.

**24.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mchango wa sekta binafsi unatarajiwa kupatikana kupitia uwekezaji katika ukuzaji mitaji, hususani katika mali za kudumu na shughuli za kiuchumi na kijamii kama vile viwanda na biashara, nishati na madini, kilimo, mifugo na uvuvi, maji, afya, elimu, utalii, mitambo, mashine, miundombinu ya uzalishaji, miundombinu ya usafiri na usafirishaji, na teknolojia.

## UFUTILIAJI NA TATHMINI KWA KUZINGATIA MATOKEO

**25.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** katika kufikia malengo ya Mpango, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa ni nyenzo muhimu za usimamizi na uwajibikaji. Hivyo basi, Serikali imeweka mfumo imara wa ufuatiliaji na tathmini utakaowezesha kukusanya na kuchakata taarifa sahihi kwa wakati ili kupima hatua zilizofikiwa katika utekelezaji kwa kuzingatia matokeo (*Results Based Monitoring, Evaluation, Learning and Accountability Framework*).

**26.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Kutakuwa na aina mbili za ufuatiliaji na tathmini, ambazo ni tathmini ya utekelezaji wa mpango kwa robo mwaka, nusu mwaka, na mwisho wa mwaka kupitia viashiria vya matokeo ya moja kwa moja (*Key Performance Indicators – KPIs*), na tathmini maalum kulingana na mahitaji.

**27.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya viashiria vya mpango wa muda mfupi na muda wa kati zitaandaliwa na kuwasilishwa Tume ya Taifa ya Mipango kupitia mfumo wa NPMIS (***National Planning Management Information System***). Kwa kuzingatia

umuhimu wa taarifa hizi katika kufanya maamuzi ya maendeleo, wakuu wa taasisi za umma watapaswa kuzingatia masuala yafuatayo:

i) Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitakuwa kigezo kikuu cha kupima utendaji wa taasisi pamoja na wakuu wa taasisi husika

ii) Tume ya Taifa ya Mipango itaandaa taarifa za jumla za ufuatiliaji na tathmini na kuziwasilisha katika vikao vya kimaamuzi, ikiwemo Baraza la Mawaziri, kwa lengo la kuwezesha kufanyika maamuzi sahihi na kwa wakati

iii) Taarifa za ufuatiliaji na tathmini zitatumika kama moja ya vigezo muhimu katika kuidhinisha utoaji wa fedha za maendeleo.

**28.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** majukumu ya ufuatiliaji na tathmini yamegawanyika katika ngazi sita zifuatazo:

i) Tume ya Taifa ya Mipango

ii) Wizara/Idara zinazojitegemea

iii) Sekretariati za mikoa

iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa

v) Wakala na Mashirika ya Umma

vi) Taasisi za Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia.

**29.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Katika sura ya saba, Kitabu cha Mpango kimeainisha vihatarishi saba vinavyoweza kuathiri kufikiwa kwa

malengo yaliyowekwa. Ili kukabiliana na vihatarishi hivyo, Mpango umeainisha misingi saba ya kuzingatia kama ifuatavyo:

i) Kuendelea kuimarisha uwezo wa utekelezaji na uratibu miongoni mwa taasisi za serikali ili serikali iweze kutekeleza mpango kama chombo kimoja (Connected Thinking, Coordinated Execution)
ii) Kuendelea kujenga uwezo wa kifedha wa kugharamia Mpango kwa kuendelea kujenga mazingira sahihi ya kufanya biashara na kukuza sekta binafsi nchini
iii) Kuendelea kujenga uwezo wa raslimali watu kama msingi mkuu wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo
iv) Kuendelea kujenga uwezo wa kuhimili na kukabiliana na mitikisiko na mdodororo wa kiuchumi duniani
v) Kuimarisha ushiriki wa sekta binafasi katika kutekeleza programu, miradi na afua zilizoainishwa katika Mpango
vi) Kuchochea mageuzi ya kidigitali katika ngazi zote
vii) Kuimarisha amani na utulivu wa kisiasa.

## HITIMISHO

**30.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Kama nilivyoeleza awali, huu ni Mpango wa kwanza katika kuanza kutekeleza Dira 2050 na Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV). Katika mpango huu tumeainisha hali ya uchumi na mwelekeo wake katika kipindi cha mwaka 2026/27. Kwa ujumla wake, hali ya uchumi ni tulivu na mweleko wake ni kuendelea kukua. Hata hivyo, hii itategemea na uwezo wetu wa kukuza mapato ya ndani na kuvutia uwekezaji ili kuepuka, kustahimili na kukabiliana na misukosuko ya uchumi duniani na mabadiliko hasi ya kijiopolitiki. Hii itahitaji kuongeza jitihada zaidi katika kurasimisha shughuli za kiuchumi na kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na kuvutia uwekezaji.

**31.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Mpango umeainisha maeneo matano ya kipaumbele kwa kuzingatia maudhui ya Mpango wa Nne wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (*FYDP IV*) na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, pamoja na maono na maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoyatoa kupitia hotuba yake ya kulifungua Bunge la 13 na hotuba zingine alizozitoa tangu alipoapishwa.

**32.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Moja ya eneo kubwa la utofauti la mpango huu ukilinganisha na mipango iliyopita ni kutambuliwa bayana kwa ushiriki na mchango wa sekta binafsi katika kufanikisha utekelezaji wa mpango huu wa maendeleo. Gharama za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2026/2027 zinakadiriwa kuwa TZS trilioni 86.3, ambapo uwekezaji wa sekta binafsi unatarajiwa kuchangia TZS trilioni 60.1 (70%), ukilinganisha na mchango wa Serikali wa TZS trilioni 20.7 (24%) kutoka katika bajeti kuu ya serikali, na TZS trilioni 5.5 (6%) kutokana na uwekezaji wa mashirika ya umma. Hivyo basi, sote tutahitaji kubadilika na kubadili mitazamo yetu kwa kujielekeza katika kuheshimu sekta binafsi na kuweka mazingira sahihi ya kukua kwake.

**33.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Aidha, ili kufanikisha utekelezaji wa mpango huu na kupata matokeo tarajiwa tutahitaji kubadilika kwa kujenga nidhamu ya **UTEKELEZAJI** wa tunayopanga bila kuyumba. Katika kufanikisha hili, tumeweka mfumo thabiti wa ufutiliaji na upimaji kwa kuzingatia matokeo (Results Based Monitoring, Evaluation, Learning and Accountability Framework), kama ulivyoanishwa katika sura ya sita ya Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango.

**34.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa ujumla wake, nyenzo zote tatu za kuanza utekelezaji wa Dira 2050 zimekamilika mapema kabla ya kuanza utekelezaji wake rasmi, kuanzia tarehe 01 Julai 2026. Nyenzo hizi ni Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Muda Mrefu (LTPP 2050), Mpango wa Nne wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (FYDP IV), na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2026/27, ambao mapendekezo yake nimewasilisha leo hapa Bungeni. Nichukue nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake thabiti ambao ulisimamia maandalizi haya kikamilifu na kuhakikisha kuwa maandalizi ya Dira 2050 na nyenzo zake za utekelezaji zitakamilika mapema ndani ya muda. Kama nilivyowahi kusema huko nyuma, hii ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kukamilisha Dira na nyenzo zake za utekelezaji kwa wakati mmoja.

**35.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Aidha, nichukue nafasi kuwashukuru wasaidizi wa karibu wa Mheshimiwa Rais, na viongozi wetu wengine wakuu, kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais pamoja na miongozo yao makini katika kusimamia utekelezaji wa mipango ya serikali na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. Hawa ni Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mbunge wa Iramba Magharibi), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa usimamizi wao makini wa shughuli za serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu umeanza kutekeleza Dira 2050 na mipango yake mapema kabisa, na tayari umeshaanza kutujengea nidhamu ya UTEKELEZAJI kupitia ziara zako mikoani ambazo zimekuwa na mafanikio makubwa na ambazo zinaacha matumaini makubwa kwa wananchi.

**36.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Ninawashukuru sana waheshimiwa mawaziri wenzangu, na wataalam wa wizara zao, kwa jinsi walivyotupa ushirikiano katika maandalizi ya mpango huu, pamoja na FYDP IV. Baada ya kupanga sasa ni UTEKELEZAJI na sote sasa tujielekeze katika UTEKELEZAJI. Nami kama waziri mwenye dhamana ya mipango, baada ya kukamilisha kwa mafanikio makubwa maandalizi ya mipango yetu ya maendeleo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, nitajielekeza katika kuratibu utekelezaji, hivyo, katika kipindi hiki cha utekelezaji wa Dira 2050 na nyenzo zake, sitokuwa tu waziri wa mipango, bali pia waziri wa utekelezaji (minister of implementation)!

**37.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, kwa ujumla wake, Serikali itaendelea kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji, tathmini na usimamizi wa miradi na

programu za maendeleo ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kwa ubora, kwa gharama stahiki na ndani ya muda uliopangwa. Aidha, juhudi zaidi zitaelekezwa katika kuongeza uwajibikaji wa taasisi zinazotekeleza miradi, kuimarisha uratibu kati ya sekta mbalimbali na kuhakikisha miradi ya kimkakati inaleta matokeo yaliyokusudiwa katika kukuza uchumi, kuongeza ajira na kuboresha ustawi wa wananchi.

**38.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** Ninapohitimisha, ninapenda kumshukuru Mhe. Dkt. Pius Stephen Chaya (Mbunge wa Manyoni), Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais – Mipango na Uwekezaji, kwa mchango wake mkubwa katika kuratibu na kusimamia maandalizi ya mpango huu. Ninampongeza Dkt. Tausi Mbaga Kida kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu– Mipango na Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango. Ninamshukuru kwa kuratibu kwa ufanisi maandalizi ya Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2026/27. Ninawashukuru Naibu Makatibu Watendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango na wataalam wao kwa ushirikiano na utaalam wao katika maandalizi ya Mpango huu. Nichukue nafasi pia kumpongeza Ndugu Sosthenes Laurent Kewe kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Katibu Mtendaji wa Tume ya Taifa ya Mipango (Ufuatiliaji na Tathmini). Hongera sana Ndugu Kewe na karibu katika utumishi wa umma.

**39.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Baada ya maelezo hayo, ninaomba Bunge lako lipokee Mapendekezo ya Serikali ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2026/27.

**40.** ***Mheshimiwa Mwenyekiti***, Ninaomba kuwasilisha.

Kitila Alexander Mkumbo (Mb.),

***Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji)***

11 Machi 2026.